


# **HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI**



**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU NG,OMBE WALIOCHINJWA KWENYE  
LORI NO. T-486 DHZ ENEO LA TEGETA KARIBU NA NJIA YA KUELEKEA  
MACHINJIONI JANA JUMAPILI TAREHE 13/05/2017 SAA 10.30 ALFAJIRI.**

Jana jumapili tarehe 13/05/2018 saa 10.30 Alfajiri , Wananchi wema walitoa taarifa kuhusu Ng,ombe waliochinjwa kwenye lori No. T-486 DHZ eneo la Tegeta karibu na barabara/njia ya kuelekea machinjioni ambapo dereva na watu waliokuwa wakiwachinja Ng,ombe hao walikimbia kutokana na kelele zilizokuwa zikipigwa na wananchi hao.

Mkaguzi wa nyama wa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni alipewa taarifa hiyo akiwa machinjioni akiendelea na majukumu yake ya ukaguzi wa nyama hivyo akalazimika kukatisha na kwenda katika eneo la tukio na kukuta wananchi wengi ambapo alichukua jukumu la kufanya mawasiliano kwa haraka na Mamlaka mbalimbali likiwemo jeshi la polisi ambao walidhibiti eneo hilo na hakuna nyama au kiungo kilichotoka au kuuzwa kama baadhi ya vyombo vya Habari vilivyopoti .


Kwa taarifa hii tunaujulisha umma kuwa Ng,ombe wote 12 waliokutwa kwenye gari wakiwa wamekufa waliteketezwa kama sheria na taratibu zinavyotutaka katika eneo la Mabwepande kwa kuchomwa moto na kufukiwa, chini ya ulinzi wa Jeshi la polosi na usimamizi wa Afisa Mifugo wa Manispaa, Afisa Afya wa Manispaa, Afisa kutoka bodi ya nyama,Afisa kutoka TFDA na Afisa wa Wizara ya Mifugo na uvuvi.

Aidha baada ya kuteketezwa kwa nyama hiyo hatua zifuatazo zimechukuliwa:-

1. Machinjio ya Tegeta imefungwa, wakati uchunguzi unaendelea na kupisha hali ya utulivu wakati wananchi wakisubiri kupata mrejesho kwa kila hatua zitakazochukuliwa.
2. Jalada la maelezo limefunguliwa .
3. Gari ili yobeba ng,ombe hao imeshikiliwa kituo cha polisi Wazo .

4. Polisi wanamtafuta Mfanyabiashara anayehusika na Ngombe hao kwa hatua zaidi za kisheria , wakati Ofisi hajatoa kibali cha kuondoa ngombe wake 42 kati ya ngombe 54.
5. Idara ya Mifugo inaendelea na ufuatiliaji wa usimamizi wa kudhibiti uchinjaji ,usitokee kwa kuwa Machinjo imefungwa.
6. Kuruhusu Ngombe walioshushwa machinjioni kupelekwa machinjio zingine ambapo 55 ziliondolewa usiku wa jana jumapili tarehe 13/05/2018 na waliosalia wameondolewa leo jumatatu tarehe 14/05/2018.
7. Kufuatilia kama Wataalamu wa mifugo , Wizara ya Mifugo na Uvuvi waliruhusu gari yenyé mifugo hiyo kituo cha ukaguzi Kibaha mizani na kwenye mnada wa Pugu.

Imetolewa na:-



Sebastian M. Mhowera

AFISA UHUSIANO WA MANISPAA.  
HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI